# OFISI YA WAZIRI MKUU
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA MJI – KOROGWE

SHULE YA SEKONDARI YA
WASICHANA KOROGWE,
S. L. P. 155,
**KOROGWE**
**11/12/2019**

*Simu: +255-27-2640541*
*Fax: +255-27-2640694*

**KUMB. Na. KGSS/A/11/12/2019**

Mwanafunzi…………………………………………

……………………………………………………

S. L. P. . ……………………………………………

…………………………………………………….

## YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA KOROGWE MWAKA 2020

**1.0.** Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha **Kwanza** katika shule hii mwaka 2020. Shule ya sekondari ya Wasichana Korogwe ipo umbali wa Kilometa mbili kutoka kituo cha mabasi cha mji mkuu wa Wilaya ya Korogwe. Usafiri wa Bajaji/taxi unapatikana katika kituo cha mabasi cha Mji wa Korogwe. Nauli ni shilingi elfu moja (Bajaji) na elfu tatu (tax).

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe ***06/01/2020*** Unatakiwa kuripoti kuanzia tarehe ***06//01/2020*** na mwisho wa kuripoti ni tarehe ***13/01/2020***

## 2.0.Mambo ya kuzingatia

### 2.1.Sare za Shule

(a)

(i). Sketi mbili rangi ya zambarau iliyokolea (kitambaa kiwe cha suti) na aina ya mshono ni rinda boksi na sketi ndefu ifike kiwiko cha mguu.
(ii). Nguo za kazi za nje. (Gauni rangi ya damu ya mzee, mshono wa marinda ya kuvuta na ndefu ifikie kiwiko cha mguu )
(iii). Sweta - rangi ya bluu ya shule ya msingi
(vi). Mashati mawili meupe ya mikono mifupi na yasiwe ya kubana.
(vii) Kwa mwanafunzi anayevaa hijabu, aje na nusu kanzu nyeupe na Hijabu nyeupe (tetron)
(viii) Viatu vyeupe jozi mbili na soksi fupi nyeupe (viatu visiwe na urembo wala kisigino kirefu)

(b). Sare ya michezo kwa shule hii ni kama ifuatavyo;

(i). T-sheti nyeupe isiyo na picha, mchoro wala maandishi
(ii). Bukta
(iii). Sketi fupi ya kuzungusha ya rangi ya kijani ya kuvaa juu ya bukta

(iv). Raba nyeupe au nyeusi

**2.3 Mahitaji Mengine**

(i) Ndoo, sahani, kijiko na kikombe.
(iii) Picha tatu za passport size (mwanafunzi awe amevaa blouse nyeupe wakati wa kupiga picha).
(iv) Koti la mvua au mwamvuli.
(v) Shuka mbili za rangi moja( light blue)
(vi) Sketi mbili za blue iliyokolea (dark blue) mshono rindabox za kuvaliwa nje ya darasa (nguo nyingine za nyumbani mwanafunzi haruhusiwi kabisa kuzivaa, hivyo asizilete) urefu ifike kiwiko cha mguu.
(vii) Taulo, malapa, mswaki, mto na nguo ya kulalia.
(viii) Track suit ya dark blue ya kujikinga na mbu wakati wa prep. usiku.
(ix) Madaftari makubwa 14, kalamu za kutosha na mathematical set moja.
(x) Nguo za ndani za kutosha.
(xi) Neti ya kuzuia mbu ya pembe nne.
(xii) Godoro moja futi mbili na nusu.
(xiii) Sanduku imara kwa ajili ya kuhifadhia vifaa vyake.
(xiv) Vitabu vya dini vya imani yake na mahitaji mengine ya dhehebu la mwanafunzi.

## 3.0 Sheria na Kanuni Muhimu za Shule

**3.1** Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria namba 26 ya mwaka 1970. Aidha inazingatia miongozo yote ya Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi;

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b). Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
(c). Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (prep.)
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa.
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
(g) Kuvaaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
(i) Mwanafunzi atakapofika shuleni awe amekata nywele na ziwe fupi njiti ya kiberiti isiweze kukaa na zisiwe zimewekwa dawa. Shuleni hakuna kusuka nywele.
(j) Kucha ziwe fupi na zisiwe zimepakwa rangi au hina.
(k) Haruhusiwi kumiliki/kuja na simu ya mkononi shuleni.

**3.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha ukafukuzwa shule**

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, Cocaine, mirungi, kubeli n. k.
5. Kupiga au kupigana

6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
7. Kudharau bendera ya Taifa
8. Kuoa au kuolewa
9. Kupata mimba, kutoa mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule
10. Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
11. Kukataa adhabu kwa makusudi.
12. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi, redio na pasi ya umeme au kifaa chochote kinachotumia umeme.
13. Kutokuhudhuria darasani pasipo sababu ya msingi.

**4.0 Mambo mengine muhimu**

(a) Medical examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.

(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

(c) Fomu ya Mzazi/Mlezi kukiri kukubaliana na sheria na kanuni za shule.

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**“KARIBU SANA KOROGWE SEKONDARI”**

**………………………**

**MKUU WA SHULE**

# PRIME MINISTERS OFFICE
# LOCAL GOVERNMENT AND REGIONAL ADMINSTRATION
# KOROGWE TOWN COUNCIL

## (B): REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**KOROGWE GIRLS**
**SECONDARY SCHOOL**
**P. O. BOX 155,**
**KOROGWE.**

**DATE………………………**

**MEDICAL OFFICER,**
**………………….. GOVN. HOSPITAL,**
**………………………………………..**
**……………………………………….**

**NAME OF PUPIL……………………………………………………………………………..**
Please examine the above named girl to ascertain her fitness for further studies.

**……………………..**
**HEADMISTRESS**

## MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by the medical officer)
I have examined the above named with regard to:
Skin……………………………………………………………………………………………….
Eyes……………………………………………………………………………………………….
Ears………………………………………………………………………………………………..
Chest………………………………………………………………………………………………
Spleen……………………………………………………………………………………………...
Abdomen…………………………………………………………………………………………..
Urine……………………………………………………………………………………………….
Stool……………………………………………………………………………………………….
Hemoglobin………………………………………………………………………………….......

**And I considered:**

1. She is good health, free from infection diseases, worms, bilharzias and fit to go to school.
2. She is now fit to return to school having treatment for………………………………………………
   ………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………….

………………………………. ………………………                ………………………
NAME AND SIGNATURE OF MEDICAL OFFICER                DATE

# OFISI YA WAZIRI MKUU
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA – KOROGWE

KOROGWE SEKONDARI
YA WASICHANA,
S. L. P. 155,
**KOROGWE.**

## (C): FOMU YA KUKUBALI NAFASI ALIYOPEWA

**SEHEMU A:** Habari za Mwanafunzi.

1. Jina kamili……………………………………………………………………………
2. Tarehe ya kuzaliwa…………………………………………………………………..
3. Wilaya alipozaliwa………………………………….. Kijiji …………………………
4. Kukubali nafasi (Ijazwe na mwanafunzi)

Mimi …………………………………………… nimeona maagizo yote ya kujiunga na shule ya Sekondari ya Wasichana Korogwe na ninakubali kutimiza masharti yote ya shule ikiwa ni pamoja na uletaji wa vifaa vinavyohitajika na kutii sheria zote za shule. Nitakapokuwa shuleni Korogwe nitajitahidi kadri ya uwezo wangu kuzingatia yote ambayo wanafunzi wanatakiwa kutimiza katika suala zima la kupata Elimu ya kujitegemea.

**Sahihi ya Mwanafunzi…………………………    Tarehe………………………..**

**SEHEMU B**: Habari za Mzazi/Mlezi (Ijazwe na Mzazi/Mlezi)

1. Jina kamili……………………………………………………………………………
2. Yeye ni Mzazi/Mlezi…………………………………………………………………
3. Kazi yake ………………………………………………………………………..
4. Anwani ya Mzazi/Mlezi
   ………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………..
5. Namba tatu za simu ikiwemo ya Mzazi/Mlezi na ndugu wa karibu wa Mwanafunzi
   (a)……………………………………………………………………………………
   (b)……………………………………………………………………………………
   (c)……………………………………………………………………………………

**UTHIBITISHO**

Mimi Mzazi/Mlezi wa ……………………………………………………….. nimehakikisha kwamba maagizo yote yemeeleweka na mtoto wangu amejaza kikamilifu sehemu A.

**Sahihi ya Mzazi/Mlezi………………………..    Tarehe…………………**